*Mulika, Juz. 44(2), 172-187*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Utumwa wa Kimaandishi na Kupuuzwa kwa Turathi Simulizi za Mwafrika: Uchunguzi Kifani wa Ukalimani wa Lugha ya Mizimu

*Titus Mpemba*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.2

**Ikisiri**

Dhana ya utumwa imezoeleka kama hali ya mtu kumilikiwa na kutumikishwa bila malipo. Hata hivyo, mtu anaweza kuwa katika utumwa wa kutawaliwa kiakili ambao haung'amuliki kirahisi kwani haudhihirishi mmiliki wala mmilikiwa. Kutokana na mfumo wa elimu ya Kimagharibi, Waafrika wameingizwa katika utumwa wa kimaandishi—aina ya kifungo cha kiakili kinachowafanya wafikiri na kupima uhalali wa maarifa kwa mizani ya ukuu wa maandishi . Mizani hiyo inayapa maandishi hadhi ya juu na kuwa kipimo cha maarifa, huku maarifa yasiyoandikwa yakionekana kuwa duni, yasiyo na uthibitisho, wala yasiyofaa kuingizwa katika mijadala ya kisayansi na kuwa kipimio cha kuelimika. Kutokana na hali hiyo, makala hii inatumia uga wa ukalimani wa lugha ya mizimu kuhoji mtazamo wa kutukuza maandishi. Utafiti huu ulifanyika mkoani Mwanza, Geita, Shinyanga, na Simiyu. Data zikikusanywa kupitia uchambuzi wa maandiko na usaili nusufunge na kuchambuliwa kimada kwa kuongozwa na nadharia za Ukuu wa Afrika, Mifumo ya Maarifa Asilia, na Ufasiri wa Kitamaduni. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa ukalimani wa lugha ya mizimu una nduni zote za ukalimani wa kisasa. Hivyo, ni ukalimani kama ukalimani mwingine. Kwa kuzingatia matokeo haya, makala hii inawashajiisha wanazuoni wa Kiafrika wabebe jukumu la kuuelimisha ulimwengu kuhusu turathi zao simulizi.

## 1.0 Utangulizi

Katika ulimwengu wa maarifa kwa ujumla, maandishi yamepewa hadhi ya juu huku maarifa yasiyo na maandiko yakionekana kuwa duni na yasiyofaa kuingizwa katika mijadala ya kisayansi kwa kuwa yanachukuliwa kuwa hayana uthibitisho. Kutokana na hali hii, maandishi yamekuwa ndiyo kipimo cha uhalali wa kuwa na maarifa au kujua jambo fulani. Mtu anayeweza kuandika na kusoma ndiye anayepewa heshima ya kuwa "mtu mwenye maarifa". Tukijikita katika uga wa ukalimani, tunaona kuwa, tangu kuibuka kwa mahitaji ya ukalimani, wakati wingi-

[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baruapepe: mpembatitus@gmail.com; titus.mpemba@udsm.ac.tz

lugha ulipozua vikwazo vya kimawasiliano kwa kuleta mkanganyiko wa lugha (Giambruno, 2008; Pöchhacker, 2004, 2016), uga huu umekua na umuhimu wake kuongezeka kwa kasi (Baker, 2011:7-8). Hata hivyo, kumeendelea kuwapo ombwe la tafiti kuhusu aina za kijadi za ukalimani, hususani barani Afrika ambako utamaduni wa kuandika ni mgeni. Kuwapo kwa hali hii kunaelezeka kihistoria.

Katika historia ya elimu barani Afrika, ukoloni haukuishia katika kudhibiti ardhi na siasa tu, bali pia ulidhibiti fikra. Kupitia elimu ya kikoloni, Waafrika walifundishwa kwamba uandishi na maandiko ndizo njia kuu za kuhifadhi na kusambaza maarifa. Kwa hivyo, turathi simulizi kama vile masimulizi ya mababu, nyimbo, methali, tafsiri za jadi za ujumbe wa kiroho, na maarifa yote yasiyoandikwa kwa ujumla zilianza kuonekana kama ujinga na ushenzi. Ni katika muktadha huo ambapo dhana ya *utumwa wa kimaandishi* inapopata uzito wake—kwa kuwa ni hali ya kiakili inayomfanya mtu awe mtumwa wa fikra za wengine bila kung’amua (Ngũgĩ wa Thiong’o, 1986; Ani, 1994; Asante, 2003; Boehmer, 2005; Mswazie & Mudyahoto, 2013).

Mbali na elimu, katika kipindi cha ukoloni, Wazungu walionesha dharau kwa mambo ya Waafrika ambayo wao hawakuyaelewa kwa kuwa hayakuzingatia vigezo vyao vya kuchunguzwa kisayansi na kuandikwa (Mswazie & Mudyahoto, 2013). Hivyo, waliyachukulia kuwa ni ya kijinga na ya kishenzi, wakawacheka Waafrika na kutumia vibaya elimu na mafundisho ya Biblia ili kuwadunisha (Clarke, 1992:xvi). Hali hii hata sasa ingalipo kwa wengi wao na imewaathiri wanazuoni wengi wa Kiafrika. Mathalani, kutokana na utamaduni huo wa Kimagharibi, wanazuoni na watafiti wengi wa Kiafrika wamekuwa wakiyatazama mambo ya Kiafrika, ukiwamo ukalimani wa lugha ya mizimu (kuanzia sasa ULUMI), kama mambo ya kishamba na yasiyofaa kutafitiwa kutokana na vikwazo vya kaida za kitamaduni, kimila na kidesturi na kukosa mashiko ya kisayansi na, hivyo, wanaona aibu kuyachunguza (Mswazie & Mudyahoto, 2013). Hali hii imesababisha Waafrika, pamoja na jamii ya wanazuoni kwa ujumla, kukosa uelewa kuhusu masuala mengi ya jadi ya Kiafrika. Matokeo yake, wamekuwa wakizionea haya na kuziepa mila zao na, badala yake, kutukuza tamaduni za kigeni, ukiwamo utamaduni wa maandishi. Katika muktadha kama huu, kuna haja ya wanazuoni wa Kiafrika kupaza sauti ili kuzisemea turathi simulizi za Kiafrika. Kwa hiyo, makala hii inajadili namna utumwa wa kimaandishi ulivyowafanya Waafrika wapuuze turathi zao simulizi na jinsi hali hiyo ilivyoathiri na inavyoendelea kuathiri tafiti katika taaluma ya ukalimani. Kwa kuchukua ULUMI kama kielelezo, makala hii inadai kuwa mifumo ya mawasiliano ya kijadi ni sehemu muhimu ya urithi dhihini wa Kiafrika unaopaswa kuchunguzwa kwa misingi ya falsafa ya Kiafrika. Lengo kuu ni kuchochea mjadala wa kitaaluma unaotambua thamani ya maarifa yasiyoandikwa kama nguzo halali ya binadamu kuuelewa ulimwengu.

Tafiti tangulizi zimeangazia ukuu wa maandishi na lugha za kikoloni, turathi simulizi kama hazina ya maarifa ya Kiafrika, uga wa ukalimani kwa ujumla, na athari ya elimu ya Kimagharibi katika kupuuzwa kwa turathi simulizi. Mathalani, dhana ya maandishi kama kipimo cha ustaarabu imekuwa na historia ndefu katika falsafa ya Magharibi. Ong (1982) anabainisha kuwa uandishi ni uteknolojishaji wa neno uliobadilisha fikra za binadamu kutoka kwenye mfumo wa masimulizi na kwenda kwenye mantiki ya kimaandishi. Vivyo hivyo, Havelock (1963) na Goody (1977) wanadai kwamba jamii zilizo na maandiko ndizo zilizoendelea kifikra na kiutamaduni. Mtazamo huu, ingawa ulijengewa hoja za kisayansi, uliweka msingi wa kuhalalisha ubaguzi wa kiutamaduni kwani ulizichukulia jamii zisizo na maandiko kuwa ni jamii zisizo na mfumo wa maarifa unaoaminika.

Wakipaza sauti zao kuhusiana na Afrika, wanazuoni kama Ani (1994, 1997) na Asante (2003) wanapinga mitazamo hiyo wakisisitiza haja ya kuangalia maarifa kwa mtazamo wa Ukuu wa Afrika[2]—yaani, kuutazama ulimwengu kwa mwono wa Mwafrika. Asante (2003) anaeleza kuwa elimu ya Kimagharibi imeweka mfumo wa Ukuu wa Ulaya[3] kama kipimo cha uhalali wa kufikiri na, hivyo, kuifanya mifumo mingine ya maarifa kuonekana kama haifai. Hali hii imewafanya Waafrika wengi waamini kuwa thamani ya maarifa inategemea iwapo maarifa hayo yameandikwa ama la. Kwa sababu hiyo, mapokeo simulizi na maarifa yote yasiyoandikwa, ukiwamo ULUMI, hayapewi uzito wa kitaaluma. Ngũgĩ wa Thiong'o (1986) anaendeleza hoja hii kwa kusema kuwa kutamalaki kwa lugha za kikoloni katika elimu na tafsiri kumechangia "ukoloni wa kifikra." Kumpokonya Mwafrika lugha yake ni sawa na kumpokonya utambulisho wake wa kiroho na kiakili. Kwa hiyo, kupuuza lugha za asili na mifumo ya mawasiliano ya jadi ni mwendelezo wa ukoloni huo. Hali hii inaelezwa zaidi katika nadharia za ukoloni mamboleo wa kimaarifa zinazoonesha namna mifumo ya elimu ilivyoendelea kuathiri namna ya kuzalisha na kuthibitisha maarifa barani Afrika (Ndlovu-Gatsheni, 2020; Mignolo, 2021).

Ama kuhusiana na turathi simulizi kama hazina ya maarifa ya Kiafrika, inaeleweka, kwa mfano, kuwa mapokeo simulizi si tu njia ya burudani, bali pia ni hazina ya elimu, maadili, na historia. Finnegan (1970) anabainisha kwamba masimulizi ni njia ya kuhifadhi kumbukumbu za kijamii na kuhakikisha mwendelezo wa maarifa. Katika jamii nyingi za Kiafrika, hekima imehifadhiwa kupitia methali, hadithi, nyimbo, na miviga ambayo hubeba maana pana ya falsafa ya maisha.

---

[2] Dhana ya Ukuu wa Afrika inatumika hapa kama tafsiri ya dhana ya Kiingereza ya *Afrocentriciy*.
[3] Dhana ya Ukuu wa Ulaya inatumika hapa kama tafsiri ya dhana ya Kiingereza ya *Eurocentrism*.

Oruka (1991), kupitia dhana yake ya "hekima ya kifalsafa"[4] anaonesha kwamba hekima ya Kiafrika haipo tu katika vitabu, bali katika akili za wazee wanaofikiri kwa undani kuhusu maisha. Vivyo hivyo, Dei (2000) na Hountondji (1997) wanasisitiza kuwa maarifa asilia[5] yanapaswa kutambuliwa kama mifumo halali ya elimu. Hata tafiti za hivi karibuni pia zinasisitiza kuwa maarifa asilia yana nafasi muhimu katika kujenga mitaala jumuishi na inayojikita katika mazingira ya jamii husika (taz., kwa mfano, Le Grange, 2020; Nakabugo, 2022). Tatizo, kama anavyoonesha Clarke (1992), ni kwamba elimu ya kikoloni ilipuuza hekima hizo na, kwa makusudi, ikaandaa mfumo wa kufundisha unaohusisha kukariri na si kufikiri.

Kwa msingi huo, mapokeo na tafsiri simulizi kama vile ULUMI vinabeba maana pana zaidi; ni lugha ya falsafa, historia, na utambulisho wa jamii. Hata hivyo, taasisi nyingi za elimu na tafiti zimekuwa zikiziona kama mambo ya kishirikina badala ya kurithishwa kama urithi wa kiutamaduni wa kipekee (Mswazie & Mudyahoto, 2013).

Pamoja na tafiti tangulizi nyingi kuangazia maeneo mbalimbali, bado kuna ombwe la uelewa kuhusiana na aina za jadi za ukalimani. Ukalimani ni uga muhimu katika mawasiliano baina ya tamaduni. Pöchhacker (2004, 2016) anaeleza historia ndefu ya ukalimani kama taaluma iliyoibuka kutokana na hitaji la kimawasiliano. Hata hivyo, tafiti nyingi zimejikita kwenye ukalimani wa kisasa wa mikutanoni, hospitalini au mahakamani, huku aina za kijadi zikifumbiwa macho. Mpemba (2015) anabainisha upungufu huu anaposema kuwa tafiti za Kiafrika zimekuwa zikitegemea zaidi mitazamo ya Kimagharibi na kusahau vyanzo vyake vya asili.

Kwa upande mwingine, tafiti chache kama za Giambruno (2008) na Baker (2011) zinaonesha kwamba ukalimani ni zaidi ya tukio la kiisimu; ni kitendo cha kitamaduni kinachohusisha ufasiri wa maana, mamlaka, na muktadha. Kutokana na hilo, ULUMI unaweza kuchukuliwa kama mfumo wa tafsiri wa kipekee unaounganisha ulimwengu wa roho na wa wanadamu kupitia ishara, sauti, na matamshi. Mfumo huu, japokuwa hauandikwi, una kanuni na taratibu mahususi zinazoukilia ufasiri wa ujumbe wa mizimu kwa binadamu na ujumbe wa binadamu kwa mizimu. Mtazamo huu unaendana na tafiti za hivi karibuni zinazouona ukalimani kama tendo la kijamii na kitamaduni linalohusisha mazungumzo, mamlaka, na uhusiano wa wahusika (taz., kwa mfano, Baraldi, 2021; Rundle, 2022).

Hata hivyo, kutokana na athari za elimu ya Kimagharibi, ukalimani huo, pamoja na turathi zingine simulizi, umefumbiwa macho na watafiti. Elimu ya Kimagharibi

[4] Hii ni tafsiri ya dhana ya Kiingereza ya *philosophic sagacity*.
[5] Hii ni tafsiri ya dhana ya Kiingereza ya *indigenous knowledge*.

imejikita katika dhana kwamba maarifa yanapaswa kuthibitishwa kwa maandiko na tafiti jaribizi. Hali hii imewafanya wanazuoni wa Kiafrika wengi kuwa waoga kuandika au kuchunguza masuala ya kitamaduni ambayo hayana vielelezo vya maandiko. Clarke (1992) anaonya kuwa huu ni mwendelezo wa "utumwa wa kifikra" unaotufanya tuzionee aibu mila zetu. Boehmer (2005) naye anaeleza kuwa ukoloni wa kiutamaduni unaendelezwa kwa njia za kitaaluma—kupitia mitaala, lugha, na vigezo vya utafiti vinavyotukuza "sayansi" huku vikibeza simulizi. Kwa muktadha huu, kuchunguza ULUMI ni kitendo cha kisayansi na cha kisiasa; ni kitendo cha kurudisha heshima ya maarifa ya Kiafrika yaliyodunishwa. Hii ndiyo hoja ya msingi ya makala hii: kwamba utumwa wa kimaandishi umepunguza upeo wa uelewa wetu kuhusu hekima simulizi za Kiafrika; na kwamba wajibu wa mwanazuoni wa Kiafrika ni kuikomboa elimu kutoka katika makucha ya vikwazo hivyo vya kupuuzwa kwake.

## 2.0 Kiunzi cha Kinadharia na Methodolojia ya Utafiti

Misingi ya kuielewa makala hii imekitwa katika nadharia tatu: Nadharia ya Ukuu wa Afrika, Nadharia ya Mifumo ya Maarifa Asilia, na Nadharia ya Ufasiri wa Kitamaduni. Nadharia ya Ukuu wa Afrika iliasisiwa na Molefi Kete Asante kunako miaka ya 1980 na kuendelezwa zaidi miaka ya 2000. Asante anasisitiza kuwa tafsiri yoyote ya maisha, maarifa, au historia ya Mwafrika haina budi kuanzia kwenye uzoefu wa Mwafrika mwenyewe; si kwenye msingi ya kigeni. Lengo kuu la nadharia hii ni kumrejeshea Mwafrika ujasiri wa kujitazama mwenyewe ambao alinyang'anywa na mkoloni, na kupinga hali ya iliyopo sasa ya kuutazama ulimwengu kupitia macho ya mkoloni. Katika muktadha wa makala hii, Nadharia ya Ukuu wa Afrika inaweka msingi wa kuutazama ULUMI kama uga wa maarifa ya kweli, yenye mantiki ya ndani na misingi ya kifalsafa ya Kiafrika. Kwa mujibu wa Asante (2003), ukombozi wa fikra ni hatua ya kwanza ya ukombozi wa kisayansi. Kwa sababu hiyo, ili kujinasua katika makucha ya utumwa wa kimaandishi, hatuna budi kufikiria upya namna tunavyopima uhalali wa maarifa.

Nadharia ya Ukuu wa Afrika inapingana na nadharia ya Ukuu wa Ulaya ambayo inachukulia kuwa njia pekee ya kujua jambo fulani ni ile inayozingatia mikabala ya Kimagharibi—maandishi, tarakimu, na uthibitisho wa kijaribizi. Badala yake, inatambua kuwa maarifa yana sura changamani na yanaweza kuishi katika nyimbo, masimulizi, au miviga ya kijamii.

Kwa hiyo, kwa kutumia kanuni ya udadisi uliokitwa katika Ukuu wa Afrika, makala hii inasisitiza kuwa ULUMI utazamwe kama tafsiri ya kifalsafa ya maisha ya jamii, inayojengwa katika maadili ya kuheshimu wahenga, maumbile, na ulimwengu wa kiroho. Kwa hivyo, tafsiri ya lugha ya mizimu si kitendo cha kishirikina wala kishamba, bali ni njia ya kuendeleza uhusiano kati ya ulimwengu wa wanadamu na ule wa kiroho—uhusiano unaoongoza uelewa wa kimaadili, kijamii, na kihistoria wa jamii inayohusika. Ikumbukwe kuwa, hata katika shughuli za kidini za kimagharibi, kuna yanayofanywa pasipo maandiko kama

ufaraguzi wa mawasiliano baina ya washiriki wa liturujia na Mungu na wale wanaotambuliwa kama watakatifu.

Kwa upande wa Nadharia ya Mifumo ya Maarifa Asilia, ambayo ni msingi wa pili wa kinadharia ulioongoza utafiti huu, kama inavyoelezwa na waasisi wake (Hountondji, 1997; Semali & Kincheloe, 1999; na Dei, 2000), nadharia hii inatambua kwamba kila jamii ina mifumo yake ya kujua na kupata maarifa ambayo inajengwa katika historia, lugha, imani, na mila zake. Maarifa haya ni hai, yanafundishwa na kurithishwa kwa vizazi vinavyofuata kupitia tajiriba na masimulizi, na hayategemei maandiko ili yaendelee kudumu. Jambo hili liko wazi sana kwa jamii nyingi za Kiafrika, ambapo uhalali wa kujua au "kuwa na maarifa" unategemea tajiriba na ushiriki wa kijamii na si uandishi. Wazee, wapiga ramli, na wakalimani wa lugha ya mizimu wamekuwa wahifadhi na wasambazaji wa maarifa kwa njia ya masimulizi na miviga. Hountondji (1997) anatahadharisha dhidi ya ulimbukeni wa kilimbwende[6] unaotaka kuyaona maarifa ya asili kama masalia ya kihistoria badala ya kuyaona kama mifumo hai ya uelewa wa dunia. Kwa hiyo, kwa mtazamo wa nadharia hii, ULUMI una maana zaidi ya uhawilishaji wa ujumbe wa mizimu. Ni kitendo cha kijamii cha kusuluhisha migogoro, kueleza na kukabili majanga, au kuimarisha maadili. Hivyo, ni sehemu ya "miundombinu ya maarifa" ya Kiafrika inayoweza kutumika katika nyanja za tafsiri, falsafa, na elimu, miongoni mwa nyinginezo.

Maarifa asilia yana kanuni zake za kimantiki ambazo, kwa mujibu wa Dei (2000), zinapaswa kuchunguzwa kwa uangalifu badala ya kulinganishwa kwa upofu na mantiki za kisayansi za Kimagharibi. Kwa mfano, pale mizimu inapozungumza kupitia kiti na mkalimani, jamii huyachukulia maelezo hayo kwa uzito sawa na hukumu ya kisheria au taarifa ya kitaalamu. Hii inaonesha kuwa uhalali wa maarifa simulizi hauhitaji uthibitisho wa maandishi bali unategemea uaminifu wa kijamii na uhusiano wa kiroho.

Nadharia ya Ufasiri wa Kitamaduni, kama ilivyoendelezwa na Homi Bhabha (1994) na Susan Bassnett (2014), inaitazama tafsiri kama tukio la mamlaka ya kitamaduni. Tukio hilo halichukuliwi kuwa ni la kiisimu pekee kwani hujumuisha tafsiri ya maana, mamlaka, na muktadha. Kila tafsiri hujenga daraja kati ya ulimwengu wa aina mbili: ulimwengu chanzi wa mtoa ujumbe na ulimwengu lengwa wa mpokea ujumbe.

Kwa kuhusisha nadharia hii na ULUMI, tunamaizi kuwa kila kitendo cha ukalimani ni uwanja wa kimamlaka kati ya ulimwengu wa mizimu na ulimwengu wa wanadamu. Mkalimani wa lugha ya mizimu ana nafasi ya kipekee: yeye ni mpatanishi anayefasiri ujumbe wa kimizimu, au ukipenda wa kiroho, kwa lugha ya

[6] Dhana hii inatumika kama tafsiri ya dhana ya Kiingereza ya *romantic primitivism*.

wanadamu bila kupoteza mamlaka ya chanzo cha ujumbe huo. Hii ni tafsiri ya kipekee ya kitamaduni ambayo inavunja mipaka ya tafsiri ya kisasa inayozingatia tu uhalisia wa maneno ya lugha ya mwanadamu.

Kwa hiyo, Nadharia ya Ufasiri wa Kitamaduni inatusaidia kuuelewa ULUMI kama tukio lenye vipengele vya mamlaka, imani, na uhalisia wa kimizimu. Katika muktadha wa makala hii, inatusaidia kuona kuwa utumwa wa kimaandishi si tu tatizo la elimu bali ni tatizo la mamlaka ya kiutamaduni—ni namna ambavyo jamii imeminywa na kunyimwa uwezo wa kujitafsiri yenyewe.

Makala hii inatumia mkabala wa ufasiri wa kitaamuli. Lengo halikuwa kupima matokeo kwa takwimu, bali kuelewa maana zilizojificha katika turathi simulizi za Kiafrika na uhusiano wake na ukalimani, hasa ukalimani wa ndimi kama vile lugha ya mizimu. Kwa kutumia mkabala huu, utafiti huu ulilenga kutoa uelewa wa kina kuhusu mikanganyiko iliyowekwa na ukoloni kwenye mifumo ya maarifa ya Kiafrika kwani mkabala huu uliruhusu uchunguzi wa kina wa namna turathi simulizi na lugha za ndimi zilivyofumbiwa macho katika muktadha wa ukalimani wa Kiafrika.

Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maandiko yanayohusiana na ukalimani na turathi simulizi za Kiafrika. Aidha, usaili nusufunge ulifanyika ambapo wazee wa Kisukuma, waganga wa jadi, wakalimani wa lugha ya mizimu, ambao ni hifadhi ya turathi simulizi pamoja na wateja wao, walisailiwa. Washiriki hawa walichaguliwa kwa mbinu ya usampulishaji taje, ambapo washiriki wa mwanzo walisaidia kutambulisha wengine wenye ujuzi wa kina kuhusu mifumo ya kimasimulizi na lugha ya mizimu ya Kisukuma. Kadhalika, data zilipatikana kupitia ushuhudiaji wa moja kwa moja uliofanyika katika maeneo ya Mwanza, Geita, Shinyanga, na Simiyu, ambapo ULUMI ni maarufu, hasa katika miviga ya kung'amua majanga yanayowasibu wateja.

Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa kutumia uchambuzi wa kimada, yaani kubaini mada zinazojitokeza kutokana na usaili na usomaji wa maandiko. Hapa, mada mahususi zilizolengwa zilikuwa nduni kuu za ULUMI na stadi kuu zinazotumika katika ukalimani huo. Nduni hizo na stadi hizo zilichanganuliwa na kulinganishwa na nduni pamoja na stadi zinazohitajika katika ukalimani wa kisasa. Lengo lilikuwa kugundua mifumo ya namna turathi simulizi za Kiafrika zinavyotazamwa kitaaluma na kitamaduni, hasa kuhusu ukalimani wa lugha za mizimu.

Kwa kuwa utafiti huu ulihusisha masuala ya imani na faragha za wateja wa waganga kama washiriki, masuala ya itikeli za utafiti yalizingatiwa kwa umakini. Washiriki walihakikishiwa kuwa majina yao yatakuwa siri na walikubali kushiriki kwa hiari yao. Aidha, walitoa ridhaa ya kushiriki kwa kuwa walielewa madhumuni

ya utafiti na haki yao ya kujitoa wakati wowote katika utafiti bila athari yoyote kwani walifahamishwa hivyo.

## 3.0 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba ULUMI una nduni sawa na zile za ukalimani wa kisasa, hasa katika muktadha wa ukalimani wa kijamii na ukalimani katika huduma za umma. Hii ni kwa sababu ukalimani wa kisasa ni shughuli ya kuwezesha mawasiliano baina ya pande mbili zinazotumia lugha tofauti, ambayo hufanyika papo kwa papo na katika mazingira yenye shinikizo la kupokea na kuchakata ujumbe chanzi na kuzalisha na kuwasilisha kwa usahihi ujumbe wa lugha chanzi kwa lugha lengwa. Vivyo hivyo, katika ULUMI, kiti wa mizimu hupokea ujumbe wa kiroho na mkalimani huukalimani kwa wateja mara moja, na huwa hana nafasi ya kuupitia wala kuusikiliza tena ujumbe chanzi. Hali hii inaufanya ULUMI kuwa tukio la papo kwa papo na linalodumu kwa muda mfupi tu, nduni kuu ambazo zinatambulika katika ukalimani wa kisasa. Mathalani, inaendana na tafiti za ukalimani wa kijamii zinazoonesha kuwa ukalimani hutegemea sana muktadha wa kijamii na mtagusano wa washiriki (Wolf, 2020; Jusufović, 2021).

Kwa ujumla, maandiko yaliyopitiwa yalibainisha nduni kuu tano za ukalimani wa kisasa. Ushuhudiaji ulionesha kuwa nduni hizo pia zinadhihirika katika ULUMI. Jedwali Na. 1 linabainisha nduni, maelezo yake na vyanzo vyake huku likionesha uhusiano wa kila nduni na ULUMI.

**Jedwali Na. 1: Nduni za Ukalimani wa Kisasa na Namna Zinavyohusiana na ULUMI**

| Na. | Nduni za Ukalimani wa Kisasa | Maelezo | Chanzo | Uhusiano na ULUMI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Upapo kwa papo | Ukalimani hufanywa papo kwa papo na kwa manufaa ya watu wanaotaka kushiriki katika mawasiliano ya kuvuka vikwazo vya lugha na tamaduni tofauti. | Kade (1968), akirejelewa na Pöchhacker (2004:10); Pöchhacker (2004:10; 2010: 154) | Matukio yote ya ULUMI yaliyoshuhudiwa yalifanyika papo kwa papo. Lengo lake—kuwezesha mawasiliano kati ya watu waliotaka kushiriki katika mawasiliano yakivushwa kwenye vikwazo vya lugha na tamaduni—lilikuwa sawa na nduni za ukalimani wa kisasa. Hata hivyo, kikwazo cha kiutamaduni kilikuwa kidogo kwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | kuwa wateja wengi walikuwa na utamaduni sawa na wa mizimu, waganga wa jadi, na wakalimani. |
| 2. | Kudumu kwa muda mfupi tu | Ukalimani hufanyika katika tukio la muda mfupi au lenye kudumu kwa kipindi kifupi. | Pöchhacker (2004:11) | Matukio yote ya ULUMI yaliyoshuhudiwa yalidumu kwa muda mfupi. Hii ilikuwa tu wakati ambapo waganga walikuwa katika hali ya kupandisha mizimu. Katika kila tukio lililoshuhudiwa, ukalimani ulikoma mara tu baada ya mzimu kuondoka |
| 3. | Kufanyika kwa wakati halisi au uliopo | Ukalimani ni tukio lifanywalo kwa wakati halisi au uliopo na binadamu walio katika muktadha wa pamoja wa kimawasiliano, ambapo wazungumzaji huzalisha matini kwa wakati huohuo. | Pöchhacker (2009:128; 2010:154); Hale (2007:128) | Matukio yote ya ULUMI yaliyoshuhudiwa yakifanyika kwa wakati halisi au uliopo. Wakalimani walikuwa wakifanya ukalimani wa matukio ya wakati uleule kwani ujumbe chanzi ulikuwa ukitoka moja kwa moja na kwa wakati uleule kwa watoa ujumbe, yaani mizimu. Kwa maneno mengine, hakuna usemi uliokalimaniwa ambao ulikuwa umerekodiwa. |
| 4. | Upatikanaji usiojirudia, yaani uwasilishaji wa mara moja tu wa ujumbe chanzi | Ujumbe wa lugha chanzi huwasilishwa mara moja tu na hivyo hauwezi kurudiwa (wala kupitiwa au kusikilizwa) tena. | Kade (1968), akirejelewa na Pöchhacker (2004:10; 2010:154); Schäfner (2004:1-2) | Mizimu husema mara moja tu. Hata hivyo, inawezekana ujumbe chanzi ukarudiwa ikiwa mkalimani wa ULUMI atakosa kuelewa jambo fulani au kama mzimu atabaini kuwa mkalimani amekosea, ambapo anaweza kuamua kurudia kwa kuwa anatambua viwango vya usahihi wa kinachokalimaniwa na hawezi kuvumilia kuona ujumbe ukipotoshwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Kutorekebishi-ka wala kurudiwa kwa ujumbe lengwa kutokana na shinikizo la muda wa uzalishaji | Ujumbe wa lugha lengwa huzalishwa katika mazingira yenye shinikizo la muda, na uwezekano mfinyu sana wa kufanya marekebisho au udurusu. | Kade (1968), akirejelewa na Pöchhacker (2004:10) | Matukio yote ya ULUMI yaliyoshuhudiwa yalifanyika katika mazingira ya shinikizo la muda na hakukuwa na fursa ya kufanya masahihisho wala marudio. Hakukuwa na muda wa kurekebisha wala kuwasiliana na upande mwingine kwa ushauri wala kutumia zana zozote za mkalimani kama kamusi, leksikoni, sarufi, orodha za istilahi wala zana za TEHAMA kama vile kongoo, kanzidata za mtandaoni, intaneti na majukwaa ya mtandaoni kwa ajili ya marekebisho kama hayo. |

**Chanzo**: Data za Utafiti

Kama Jedwali Na. 1 linavyoonesha, ULUMI ni ukalimani kwa kuwa una nduni zote za ukalimani wa kisasa, ingawa haujulikani sana katika kilongo cha wataalamu wa ukalimani. Upekee wa ULUMI ni kwamba hufanyika katika mazingira halisi yasiyohitaji matumizi ya teknolojia za kisasa kama vile maikrofoni, seti za visikilizio vya masikioni au vya kuvaa kichwani, wala vipaza sauti. Kadhalika, hakuna haja ya mkalimani wa lugha ya mizimu kuwa na kalamu wala daftari kwa kuwa ULUMI hauhitaji uandishi wa kumbukumbu.

Mbali na kufanana kwa nduni za ukalimani wa kisasa na ULUMI, matokeo ya utafiti huu yanaonesha pia kwamba stadi zinazohitajika katika aina hizo za ukalimani zinafanana kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, katika ULUMI, mkalimani anahitaji kufanya maamuzi ya haraka, kuwa na umahiri wa lugha ya mizimu na lugha lengwa, na kuwa na uwezo wa kutoa kwa usahihi ujumbe wa lugha chanzi katika lugha lengwa. Hali hii ni sawa na ilivyo katika ukalimani wa kisasa. Tofauti iliyopo tu ni kwamba ULUMI hufanyika bila teknolojia yoyote ya kisasa, kama vile kompyuta au visikio vya sauti.

Pia, wakalimani wa lugha ya mizimu hawana budi kuwa na kumbukumbu nzuri kwani hawana nafasi ya kuandika maelezo. Wakalimani hutumia kumbukumbu isiyodumu ya kile kilichosemwa na kiti cha mizimu. Hali hii pia ni sawa na stadi za ukalimani wa kisasa ambapo mkalimani anahitaji kumbukumbu nzuri ili

kufikisha ujumbe bila kutegemea nyaraka. Hata hivyo, ukilinganishwa na ukalimani wa kisasa, ULUMI unakuwa mgumu zaidi kwa sababu unahitaji ufahamu wa kina wa tamaduni na imani za jadi zinazohusiana na jamii husika. Hii inafanya ukalimani wa mizimu kuwa na changamoto kubwa ya kufasiri ujumbe wa ulimwengu wa kiroho bila kupoteza maana au hekima ya kifalsafa inayohusiana na jamii inayohusika.

Stadi zingine zinazohitajika katika ULUMI ni ujuzi wa kukabiliana na hali za hadhira, uwezo wa kudhibiti vizuri vidato na mikazo ya sauti, na uwezo wa kufanya maamuzi ya haraka katika kufasiri ujumbe wa ulimwengu wa kiroho. Hivi ni kusema kwamba wakalimani wanapaswa kuwa na utulivu mzuri wa sauti, kuielewa kwa kina hadhira na tasnia yao, na uwezo wa kuwasilisha ujumbe kwa haraka bila kupoteza maana. Stadi hizi hazitofautiani na zile zinazohitajika katika ukalimani wa kisasa, ambapo mkalimani anahitaji kuwa na sauti nzuri, utulivu mzuri wa sauti, na uwezo wa kutoa ujumbe kwa haraka na kwa usahihi.

Kwa ujumla, kutokana na usaili, stadi lukuki zilibainishwa. Stadi hizo ziligawanywa katika makundi matatu: stadi za kuelewa ujumbe, stadi za kukumbuka, na stadi za kuwasilisha ujumbe katika lugha lengwa. Jedwali Na. 2 linaonesha stadi hizo kwa muhtasari.

**Jedwali Na. 2 Baadhi ya Stadi Zinazohitajika katika ULUMI na Ukalimani wa Kisasa**

| **Stadi Kuu** | **Stadi Ndogondogo** |
|---|---|
| *Stadi za kuelewa ujumbe* | **Stadi za kupokea na kufuma upya ujumbe (usasanyuzi na usasanyaji)**<br>*Kuyudegeleka witegelejaga* (kusikiliza kwa makini): Uwezo wa kuzingatia na kusikiliza kwa umakini |
| | *Kuyudegeleka usolanyha ishitulo* (kusikiliza huku ukibaini hoja kuu): Uwezo wa kusikiliza kiteuzi ili kutambua na kubainisha hoja kuu, kutenganisha mawazo ya msingi na ya ziada, na kuondoa uradidi |
| | *Kujeelelwa imbisila ja nyaganga* (kuelewa namna fiche za uzungumzaji wa kiganga): Uwezo wa kuelewa njia za mawasiliano za waganga wa kiroho |
| | *Kuyusolanyha wadiilila imihayo iyabhulongeke* (kuchagua na kuzingatia maneno muhimu): Uwezo wa kuchagua na kuzingatia taarifa muhimu |
| | *Kuyugamana amakulu ga mihayo nulu giibisile* (kujua maana za kile kinachosemwa hata kama zimefichwa): Uwezo wa kudokeza maana kupitia muktadha na masuala ya ziada ya lugha |
| | *Kubinzagula iyoyilihayiwa bhohalumolumo; biya kuloondela kamhayo kamokamo* (kuvunjavunja taarifa za jumlajumla; hapana kufuatilia neno moja moja): Uwezo wa kugawanya taarifa katika vipengele vya maana |
| | *Kumana mbika na mbika ja makikalile ga bhanhu ba mahanga na mahanga* (kujua aina na aina za tamaduni za jamii mbalimbali): Uwezo wa kuwa na maarifa ya msingi, ikiwa ni pamoja na maarifa ya dunia na ya mada inayozungumziwa |
| *Stadi za kukumbuka* | *Kuleka kwiibha* (kuachha kusahau): Uwezo wa kudumisha taarifa katika kumbukumbu ya muda mfupi na mrefu |

| | |
|---|---|
| *Stadi za kuwasilisha ujumbe katika lugha lengwa* | **Stadi za usahihi**<br>*Kuyutungilija akayombele na kuyulondeja shikong'wa shamushilaka kukoma umhayo gugolologe na amakulu gamaanike* (kusema kwa usahihi kulingana na mapumziko ya sauti ili ujumbe ufike moja kwa moja na maana iwe wazi): Uwezo wa kutoa toni sahihi na matumizi ya ishara za sauti ili ujumbe ujitokeze kwa usahihi na maana iwe wazi |
| | *Kuyomba yang'hana dudu; yaya kulemba nulu kulembekeja* (kusema ukweli daima; hapana kudanganya wala kusingizia): Uwezo wa kuwasiliana kwa usahihi |
| *Stadi za uwasilishaji ujumbe* | **Stadi za kuwasilisha mawazo kwa uwazi na kwa ufupi**<br>*Kuyushookeela ishitulo* (kurudia hoja muhimu): Uwezo wa kurudia hoja muhimu kwa uwazi na kwa ufupi |
| | *Kugoloola shilaka; ahakuhamuka wahamuka na ahakucheeja wacheeja* (kusawazisha sauti; pale panapohitaji kupaza sauti, unapaswa kupaza sauti, na pale panapohitaji kupunguza sauti, unapaswa kufanya hivyo): Uwezo wa kudhibiti sauti yako |
| | *Kuyuhamuka/kuyaanilija na kuyufumbula imihayo; bhiya kuhwehweta* (kusema kwa sauti na kufichua maneno; hapana kunong'ona): Uwezo wa kusema kwa sauti mwafaka na kwa uwazi |
| | *Kugoloola imihayo; biya kuyushokeelashokeela bul'ikanza* (kwenda moja kwa moja kwenye hoja na si kurudiarudia kila wakati): Uwezo wa kuwasiliana kwa uwazi na uwiano wa sauti bila kusita, kurudiarudia au kufanya marekebisho yasiyohitajika mara kwa mara |
| | *Kukaangilija utiz'untindika unyombi* (kuharakisha ili kupunguza uwezekano wa kumcheleweshа mzungumzaji): Uwezo wa kuwa na kasi inayotakiwa ili kukidhi matarajio ya mzungumzaji |

**Chanzo**: Data za Utafiti

Data katika Jedwali Na. 2 zinazidi kuthibitisha kuwa hakuna tofauti za msingi baina ya ULUMI na ukalimani wa kisasa kwa kuwa stadi zinazohusika kote zinashabihiana.

## 4.0 Mjadala

Matokeo ya utafiti huu yanathibitisha kwamba ULUMI una nduni na unatumia stadi zinazofanana na zile za ukalimani wa kisasa. Kwa hiyo, tukiongozwa na Nadharia ya Mifumo ya Maarifa Asilia, tunaweza kutetea kwa nguvu zote kuwa ULUMI ni aina ya ukalimani, lakini ambayo inakumbwa na changamoto ya kutotambulika rasmi katika vilongo vya kianazuoni, hasa katika uga wa ukalimani. Swali la kujiuliza ni, "Je, kwa nini ULUMI hautambuliwi kama ukalimani katika vilongo vya ukalimani? Swali hili, kama anavyosema Mpemba (2018), linaweza kujibiwa kwa namna mbili.

Kwanza, inawezekana kwamba wataalamu wa ukalimani hawajawahi kukutana na aina hii ya ukalimani na, hivyo, ULUMI unaweza kuwa eneo jipya linalohitaji kuchunguzwa zaidi na kujadiliwa zaidi katika muktadha wa kitaaluma. Pili, inawezekana mwelekeo wa tafiti za ukalimani kutawaliwa kwa kiasi kikubwa na mkabala wa Ukuu wa Ulaya umeathiri mtazamo wa wataalamu wa uga huo. Kwa

hivyo, bila kutarajia au kwa makusudi, wameamua kusikia na kuendeleza mawazo ya upande mmoja wa Magharibi.

Ulimwenguni tulimo sasa munatukuzwa maandishi na kubagua baadhi ya lugha na tamaduni. Kimahususi, lugha na tamaduni za asili ya Afrika zinachukuliwa kuwa ni duni au hazifai. Hii ni kwa sababu vigezo vinavyotumika kutolea hukumu ni vya uanazuoni wa Kimagharibi ambavyo vinapuuzilia mbali turathi simulizi, hasa za Kiafrika. Kama historia ya elimu ya kikoloni ilivyoonesha, lugha za kigeni na maandiko vimekuwa ndivyo vipimo vya uhalali wa maarifa na ujuzi, huku turathi simulizi za Kiafrika zikichukuliwa kuwa ni masalia ya ujinga. Hii imesababisha kupuuzwa kwa lugha za ulimwengu wa kijadi wa kiroho kama zile za mizimu, ambazo ni sehemu muhimu ya urithi dhihini wa Kiafrika. Tafiti za karibuni zinaonesha kuwa turathi simulizi zinapaswa kutazamwa kama mifumo kamili ya epistemolojia inayobeba historia, falsafa, na utambulisho wa jamii (taz. Falola, 2022). Suala hili linafafanuka vizuri zaidi kwa kutumia Nadharia ya Mifumo ya Maarifa Asilia, Nadharia ya Ufasiri wa Kitamaduni, na Nadharia ya Ukuu wa Afrika.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mifumo ya Maarifa Asilia na ya Ufasiri wa Kitamaduni, tafsiri za wenyeji na maarifa asilia vinapaswa kutambuliwa kama mifumo halali ya elimu. Hata hivyo, mkakati wa 'utengaji'[7], ambao wakoloni waliutumia kuzitenga tamaduni za watawaliwa pamoja na maarifa yanayohusiana nazo kuwa ni za kishenzi, umesababisha kutotambuliwa kwa aina hii ya ukalimani, na hii imewafanya wakalimani wa lugha ya mizimu kukosa kutambuliwa rasmi. Hata hivyo, kadiri ya matokeo ya utafiti huu, stadi za ukalimani wa lugha ya mizimu ni muhimu na zinapaswa kutambuliwa kama sehemu ya ugunduzi wa maarifa asilia ya Kiafrika katika uga wa ukalimani.

Kupitia jicho la Ukuu wa Afrika, Asante (2007:4) anasisitiza kwamba Wazungu wamekuwa wakinufaika kipekee na mfumo uliopo katika masuala ya kianazuoni, na Waafrika wamekuwa wakionekana kama wapokeaji fufumavu wa dhana, nadharia, violezo na mbinu za Kimagharibi. Hivyo, alfabeti anayotumia Mwafrika kwa kiasi kikubwa ni ya Kilatini; falsafa yake ni ya Kigiriki; nadharia na violezo anavyotumia pamoja na tafsiri zake ni za Kimagharibi na anafuata mifumo ya elimu ya Kimagharibi; hata tukiangalia filamu za Magharibi, kusikiliza nyimbo za Magharibi na kucheza michezo ya Magharibi. Kwa hiyo, walichokifanya Wazungu, na ambacho wanakifanya hadi leo, ni kuimarisha mtazamo wa kwamba Wamagharibi ndio nguvu inayoongoza duniani katika nyanja zote za maisha (Boehmer, 2005:1). Wanajiona kuwa ni mashujaa wasio na mpinzani na kila kitu chao ndicho kipimo cha ubora na upekee (Boehmer, 2005:24). Mathalani, popote pale walipoingia, walianzisha makoloni na kutangaza mwanzo wa historia mpya.

[7] Dhana hii inatumika kama tafsiri ya *othering*.

Historia zingine zilitangazwa kuwa ni duni au, katika hali fulani, zisizokuwapo (Boehmer, 2005:24).

Hali ya mambo inayoelezwa na Asante na Boehmer bado inaendelea katika mitazamo ya Wanaukuu wa Ulaya. Katika mifumo ya uchambuzi kwa mitazamo hiyo, kile kilichoandikwa ndicho kinachukuliwa kuwa cha kweli, cha kuaminika, na bora. Kwa kuwa lugha ya mizimu ya Waafrika ni ya kulongwa tu, inaonekana kuwa duni na isiyo na maana. Hivyo, haishangazi kuona kwamba, ingawa ULUMI unakidhi vigezo vyote vinavyotumika katika kufasili ukalimani, hautambuliwi kama ukalimani. Kwa mtazamo wa Wanaukuu wa Ulaya, aina hii ya ukalimani inahesabika kuwa haipo kabisa au kuwa jambo lenye umuhimu mdogo. Kwa hiyo, kwa jicho la Ukuu wa Afrika, tunaweza kudai kuwa Wazungu, na wafuasi wao, wana aina zao za ukalimani zinazokubalika kwao na, huenda hawajisikii vizuri kupanua wigo na kuruhusu aina zingine, hasa zile wanazoona kuwa ni duni, kuwa sehemu ya kapu la ukalimani. Mtazamo huu unafungamana vizuri sana na mawazo ya washiriki wa utafiti, ambao walisisitiza kuwa maarifa yaliyohifadhiwa katika turathi simulizi, kama ULUMI, si tu halali, bali pia yanafumbata ufahamu wa kifalsafa wa jamii za Waafrika. Hata hivyo, kwa kuwa turathi hizo hazina maandiko, umhimu wake katika ulimwengu wa kianazuoni umekuwa mdogo.

## 5.0 Hitimisho

Lengo la makala hii lilikuwa kujadili namna utumwa wa kimaandishi ulivyowakengeusha na unavyoendelea kuwakengeusha Waafrika katika turathi zao simulizi na kujikuta wakizipuuza na jinsi hali hiyo ilivyoathiri na inavyoendelea kuathiri tafiti za uga wa ukalimani, ikijikita katika ULUMI kama kielelezo. Dai kuu lililoendelezwa katika makala hii ni kuwa mifumo ya mawasiliano ya kijadi ni sehemu muhimu ya urithi dhihini wa Kiafrika ambao hauna budi kuchunguzwa kwa misingi ya falsafa ya Kiafrika. Mathalani, matokeo ya utafiti yameonesha kufanana kwa nduni na stadi za ULUMI na zile za ukalimani wa kisasa, hali ambayo inatupa ujasiri wa kudai kuwa ULUMI ni ukalimani kama ulivyo ukalimani mwingine. Hivyo, utafiti huu unathibitisha kuwa usimulizi si udhaifu kwani hufumbata maana zilizojificha katika maisha na falsafa za jamii.

Hata hivyo, kwa kuwa uchunguzi katika uga huu haufanyiki kwa misingi ya falsafa ya Kiafrika kutokana na kutawaliwa na mtazamo wa Ukuu wa Ulaya unaotukuza maandishi, ukalimani huo haujitokezi katika vilongo vya wanazuoni wa ukalimani, kama ilivyooneshwa katika mjadala. Matokeo yake, wataalamu wengi, na watu wa kawaida kwa ujumla, hawaujui ukalimani huo. Ili kuwawezesha kuujua na kuuelewa ukalimani huo pamoja na turathi nyingi za Kiafrika zilizo katika masimulizi, makala hii inatoa wito kwamba, badala ya wanazuoni kuzionea haya turathi hizo, wazifanyie uchunguzi zaidi na kuuelimisha

ulimwengu kuhusu turathi hizo. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wanachangia katika vilongo vya maarifa ya dunia na kupiga vita utumwa wa kimaandishi.

**Marejeleo**

Ani, M. (1994) *Yurugu: An African-centered Critique of European Cultural Thought and Behavior*. Trenton & Asmara: Africa World Press Inc.

Ani, M. (1997) *Let the Circle Be Unbroken: The Implications of African Spirituality in the African-American Experience*. Trenton: Africa World Press.

Asante, M.K. (2003) *Afrocentricity: The Theory of Social Change*. Chicago & Illinois: African American Images.

Asante, M.K. (2007) *An Afrocentric Manifesto*. Cambridge: Polity Press.

Baker, M. (2011) *In Other Words: A Coursebook on Translation*. Tol. la 2. London/New York: Routledge.

Baraldi, C. (2021) *Interpreting as Interaction: Interpreting in Intercultural Contexts*. London & New York: Routledge.

Bhabha, H. (1994) *The Location of Culture*. London & New York: Routledge.

Boehmer, E. (2005) *Colonial and Postcolonial Literature*. Tol. la 2. Oxford & New York: Oxford University Press.

Clarke, J.H. (1992) "Introduction by John Henrik Clarke". Katika Ani, M. (Mh.) (1994) *Yurugu: An African-centered Critique of European Cultural Thought and Behavior*. Trenton & Asmara: Africa World Press Inc. kur. xv-xvii.

Falola, T. (2022) *African Knowledges and Epistemologies*. Cham: Palgrave Macmillan.

Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa*. Oxford: Oxford University Press.

Giambruno, C. (2008) "The Role of the Interpreter in the Governance of Sixteenth and Seventeenth-century Spanish Colonies in the "New World": Lessons from the Past for the Present". Katika Valero-Garces, C. & Martin, A. (Wah.) *Crossing Borders in Community Interpreting: Definitions and Dilemmas*. Amsterdam & Philadelphia: John Benjamins Publishing Company. kur. 27-50.

Hale, S.B. (2007) *Community Interpreting: Research and Practice in Applied Linguistics*. New York: Palgrave Macmillan.

Havelock, E.A. (1963) *Preface to Plato*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Hountondji, P.J. (1997) *African Philosophy: Myth and Reality*. Tol. la 2. Bloomington: Indiana University Press.

Jusufović, K. (2021) "Community Interpreting and the Dynamics of Power". *Translation and Interpreting Studies*, Juz. Na. 16(2): 210–228.

Le Grange, L. (2020) "Indigenous Knowledge and Decolonising the Curriculum". *Studies in Philosophy and Education*, Juz. Na. 39(6): 603–615.

Mignolo, W. D. (2021) *The Politics of Decolonial Investigations*. Durham & London: Duke University Press.

Mpemba, T. (2015) "On Defining Interpreting and Translation: An Ordinary Language and Terminological Analysis of the Current Meanings of Kiswahili Terms Ukalimani and Tafsiri". *Journal of Linguistics and Language in Education*, Juz. Na. 9(1), 1-31.

Mpemba, T. (2018) "Spirit Medium Language Mediation: A Neglected Form of Interpreting?" *JULACE: Journal of the University of Namibia Language Centre*, 2(2), Juz. Na. 123-144.

Mswazie, J. & Mudyahoto, T. (2013) "Africanizing the Curriculum: An Adaptive Framework for Reforming African Education Systems". *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies (JETERAPS)*, Juz. Na. 4(1):170-177.

Nakabugo, M. G. (2022) "Indigenous Knowledge in African Education Systems". *International Review of Education*, Juz. Na. 68, 115–134.

Ndlovu-Gatsheni, S. J. (2020) *Decolonization, Development and Knowledge in Africa*. London & New York: Routledge.

Ngũgĩ wa Thiong'o (1986) *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. London: James Currey.

Ong, W.J. (1982) *Orality and Literacy: The Technologizing of the Word*. London: Routledge.

Oruka, H.O. (1991) *Sage Philosophy: Indigenous Thinkers and the Philosophy of the Future*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Pöchhacker, F. (2004) *Introducing Interpreting Studies*. Tol. la 1. New York & Canada: Routledge.

Pöchhacker, F. (2009) "Issues in Interpreting Studies". Katika Munday, J. (Mh.) *The Routledge Companion to Translation Studies*. London & New York: Routledge. kur. 128-140.

Pöchhacker, F. (2010) "Interpreting Studies". Katika Gambier, Y. & van Doorslaer, L. (wah.), *Handbook of Translation Studies* (Juz. 1, kur. 158-172). Amsterdam & Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.

Pöchhacker, F. (2016) *Introducing Interpreting Studies*. Tol. la 2. New York & Canada: Routledge.

Rundle, C. (2022) "Translation and Ideology in Contemporary Contexts". *The Translator*, Juz. Na. 28(1): 1–15.

Schäffner, C. (2004) "Researching Translation and Interpreting". Katika Schäffner, C. (Mh.) *Translation Research and Interpreting Research: Traditions, Gaps and Synergies*. Clevedon, Buffalo & Toronto: Multilingual Matters Ltd. kur. 1-9.

Wolf, M. (2020) *The Sociology of Translation and Interpreting*. Amsterdam & Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.